**MTIHANI WA DARASA LA NNE MUHULA WA PILI-2018**
**KISWAHILI**

Muda: Saa 1 dakika 40

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.**

Sauda ____1____ uchungu kwenye kichwa ____2____ . Alikuwa akitoka katika kanisa ____3____ lilikuwa mbali na kwao. Kichwa kilipozidi, aliketi ____4____ ya mti ili aepuke jua ____5____. Alianza kuuona mti ____6____ ukizunguka na mara akaanguka na kuzimia. ____7____, alijipata ____8____ akitibiwa na ____9____. Harufu ya ____10____ za pale ilimfanya atake kutapika. Alipotaka kuinuka, aliona miguu ____11____ ikiwa na bendeji. Hakuelewa chanzo ____12____ cha mambo ____13____ mabaya. ____14____ macho kumwomba Mungu ampe afya ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. alisikia | B. aliona | C. alihisi | D. alipata |
| **2.** | A. chake | B. pake | C. mwake | D. yake |
| **3.** | A. ambaye | B. ambayo | C. ambacho | D. ambalo |
| **4.** | A. nyuma | B. chini | C. mbele | D. juu |
| **5.** | A. makali | B. mkali | C. kali | D. vikali |
| **6.** | A. ule | B. ile | C. yale | D. mle |
| **7.** | A. Alipofufuka | B. Alipozirai | C. Alipokufa | D. Alipoamka |
| **8.** | A. shambani | B. kanisani | C. hospitalini | D. sebuleni |
| **9.** | A. marubani | B. madaktari | C. wakulima | D. wageni |
| **10.** | A. sindano | B. chupa | C. dawa | D. madawa |
| **11.** | A. yote | B. zote | C. vyote | D. chote |
| **12.** | A. vikuu | B. mkuu | C. kuu | D. kikuu |
| **13.** | A. hayo | B. huyo | C. hao | D. zile |
| **14.** | A. Alifuba | B. Alifumba | C. Alifuga | D. Alifunga |
| **15.** | A. jema | B. mbovu | C. mzuri | D. nzuri |

**Kuanzia nambari 16 hadi 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.**

**16.** Mtu akifanya jambo zuri ataambiwa:-
A. tafadhali B. samahani
C. asante D. hongera.

**17. Andika sentensi hii katika wingi.**
Shati langu limepotea.
A. Shati zetu zimepotea.
B. Mashati yangu yamepotea.
C. Mashati yetu yamepotea.
D. Shati zangu zimepotea.

**18. Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha sentensi hii.**
Kamba zilizokatika ni ______?
A. mangapi B. ngapi
C. lini D. hii


**19. Andika akisami hii kwa maneno:** $\frac{3}{5}$
A. Humusi tatu B. Thuluthi tano
C. Thumni tatu D. Ushuri tano

**20.** Jua huchomoza Mashariki na ______ Magharibi.
A. kulala B. kupotea
C. kutua D. kuzimia

**21. Gari letu hukwama barabarani.**
Huu ni wakati gani?
A. Ujao B. Mazoea
C. Ulipo D. Timilifu

**22.** Mfuko wa kuuwekea mto huitwa:-
A. foronya B. kinu
C. kochi D. shubaka.

**23.** Taja jina la umbo hili.



A. Duara B. Mraba
C. Mstatili D. Pembe tatu

**24.** Mlevi aliyekuwa katikati ______ barabara aligongwa na pikipiki.
A. na
B. mwa
C. kwa
D. ya

**25.** Chagua kinyume cha kitenzi **jenga.**
A. Bomoa
B. Jengua
C. Ujenzi
D. Usijenge

**26. Kamilisha kwa wakati unaofaa.**
Alfajiri → Asubuhi → ______
A. Alasiri
B. Jioni
C. Adhuhuri
D. Usiku

**27. Kamilisha kitendawili kifuatacho.**
Mama nieleke:-
A. mgongo
B. mtoto
C. kitanda
D. blanketi.

**28.** Kifaa cha kukunia nazi huitwa:-
A. buli
B. seredani
C. mbuzi
D. bilauri.

**29. Bainisha nomino katika sentensi ifuatayo.**
Mtoto mchanga anafaa kulala kila saa.
A. Mtoto
B. Anafaa
C. Mchanga
D. Kila saa

**30.** Chagua sentensi sahihi.
A. Shati nyeusi limeraruka.
B. Chawa kubwa amekufa.
C. Nimekula chakula tamu sana.
D. Jembe jipya hulima vizuri.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Pendo aliamka asubuhi na mapema kwa furaha nyingi. Hii ni kwa sababu siku hiyo angepelekwa kutembea kwenye mbuga ya wanyama ya Nairobi. Hiyo ingekuwa mara yake ya kwanza kuingia mbugani kuwaona wanyamapori. Baba yake alikuwa amemwahidi kumpeleka huko kama angepita mtihani wake vizuri.

Baada ya kuoga na kula, Pendo na wazazi wake waliingia garini na safari ikang'oa nanga. Haikuwachukua muda mrefu kufika kwenye mbuga. Walikuwa wakiishi karibu na mbuga hiyo.

Kwanza walienda kwenye sehemu iliyokuwa na nyoka wa aina tofauti tofauti. Pendo alimuona nyoka mkubwa aitwaye chatu. Pendo aliona kitu kama milima kwa mbali na akauliza milima hiyo iliitwaje. Baba yake alimweleza kuwa hao walikuwa ndovu. Baada ya hatua chache, nyati walijitokeza watatu. Upande mwingine waliwaona pundamilia waliopendeza sana.

Hatimaye walirudi nyumbani kwa furaha nyingi. Pendo aliwashukuru wazazi wake kwa kumpeleka mbugani. Aliahidi kufanya bidii zaidi shule zikifunguliwa.

**31.** Siku hiyo pendo aliamka akiwa na:-
- A. woga
- B. kisirani
- C. huzuni
- D. furaha.

**32.** Wazazi wa Pendo waliahidi kumpeleka mbugani kama:-
- A. angepita mtihani
- B. angewaona wanyama
- C. angeamka mapema
- D. angeanguka mtihani.

**33.** Pendo alitarajia kuona nini mbugani?
- A. Samaki mbalimbali.
- B. Miti ya kupendeza.
- C. Mimea iliyopandwa.
- D. Wanyamapori.

**34.** Pendo alipooga alikula chakula gani?
- A. Chamcha
- B. Chajio
- C. Kiamshakinywa
- D. Kishuka

**35.** Kwa nini safari ya kwenda mbugani ilikuwa fupi?
- A. Babake Pendo aliendesha gari kwa haraka.
- B. Magari yalikuwa machache njiani.
- C. Pendo waliishi karibu na mbuga.
- D. Hawakutaka kuchelewa.

**36.** Ni watu wangapi waliokuwa kwenye gari wakielekea mbugani?
- A. Wawili
- B. Watatu
- C. Wanne
- D. Moja

**37.** Pendo walitangulia kwenda sehemu gani pale mbugani?
- A. Kumwona ndovu.
- B. Sehemu iliyokuwa na nyoka.
- C. Kuwatazama ndege tofauti.
- D. Kuwafurahia pundamilia.

**38.** Wanyama waliomshangaza Pendo kwa ukubwa wao ni :-
- A. twiga
- B. ndovu
- C. vifaru
- D. kiboko.

**39.** Ni wanyama gani ambao hawakutajwa kwenye ufahamu?
- A. Nyati
- B. Pundamilia
- C. Ndovu
- D. Swara

**40.** Baada ya ziara, Pendo aliwahidi wazazi wake kufanya:-
- A. bidii shuleni
- B. mchezo shuleni
- C. fujo shuleni
- D. uzembe shuleni.

***Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali 41-50.***

Kuna misimu tofauti tofauti katika nchi yetu ya Kenya. Msimu ni mabadiliko ya hali ya hewa au anga. Kuna misimu kama ya masika, kipupwe, vuli na kiangazi. Misimu hii huletwa au kusababishwa na mvua, jua kali na baridi kali. Mvua inapokuwa nyingi hyuwa ni msimu wa masika. Jua lilikwaka kwa muda mrefu ni kiangazi na wakati wa baridi kali ni kipupwe.

Katika msimu wa masika, mvua nyingi hunyesha na kuleta furaha. Wanaofurahi zaidi ni wakulima. HIi ni kwa sababu wanapata nafasi ya kupanda mbegu na mimea tofauti. Mimea hiyo hutumia maji ya mvua ili kukua vizuri. Baadaye watu huvuna na kupata chakula cha kutosha. Chakula hiki hufanya afya za watu kuwa nzuri na wenye nguvu.

Baridi inapokuwa nyingi zaidi huitwa kipupwe. Msimu huu ni hatari kwa sababu watu wakipigwa na baridi wanaweza kuwa wagonjwa. Ili kuepuka baridi, tunafaa kuvaa nguo nzito kama vile sweta. Sehemu yoyote ya mwili haifai kuachwa wazi. Wakati wa kulala tunafaa kujifunika kwa mablanketi mazito ambayo hayataruhusu baridi kutufikia.

Kiangazi huwa msimu wenye joto jingi. Joto hili hutokana na jua kali linalowaka kwa siku nyingi. Katika kiangazi, si rahisi kuona hata tone la maji ya mvua. Huu ndio msimu mzuri wa wakulima kuvuna mazao yao shambani ili yakauke. Jua kali pia linaweza kufanya mimea kukauka kabla ya wakati wake. Hivyo basi tunafaa kuwa tayari kwa msimu wowote ili tusipate matata.

**41.** Mabadiliko ya hali ya hewa au anga huitwa:-
A. nchi B. mvua
C. vuli D. misimu.

**42.** Msimu wa masika huwa na:-
A. mvua nyingi
B. baridi kali
C. mawingu mengi
D. vumbi.

**43.** Ni kitu gani ambacho hakisababishi misimu?
A. Baridi B. Jua
C. Upepo D. Mvua

**44.** Mvua inaponyesha huleta furaha kwa wakulima kwa sababu:-
A. mimea huwa tayari kuvunwa
B. wanapata fursa ya kupanda mbegu
C. wanaweza kuvaa nguo nzito
D. wanaanza kuvuna mazao yao

**45.** Mimea hutumia _____ ili kukua vizuri.
A. baridi
B. jua kali
C. mawingu
D. maji ya mvua

**46.** Katika msimu wa kipupwe, watu wanafaa kuvaa nini?
A. Nguo nyepesi.
B. Kanzu pekee.
C. Mablanketi mazito.
D. Nguo nzito.

**47.** Joto jingi la kiangazi hutokana na:-
A. mvua kadogo B. mvua nyingi
C. jua kali D. mawingu.

**48.** Ni kitu gani ambacho si rahisi kupatikana katika msimu wa kiangazi?
A. Vumbi B. Tone la mvua
C. Jua kali D. Joto

**49.** Jua kali linaweza:-
A. kufanya mimea ikue haraka
B. kuongeza maji ya mvua
C. kuleta ugonjwa wa baridi
D. kukausha mimea kabla ya wakati wake.

**50.** Tunafaa kuwa tayari kwa msimu wowote ili:-
A. mvua iongezeke
B. tujifunike blanketi
C. tusipate matata
D. tuvae sweta.